# Mchango wa Tanzu za Asili katika Riwaya ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*

Grace Henry


## Ikisiri

*Jamii ya kijadi ya Kiafrika ilikuwa na fasihi yake kabla ya ujio wa wageni na kabla ya athari za ujio huo kama vile maandishi na kadhalika. Kutokana na kuwapo kwa tanzu za asili, tanzu za kijadi/fani simulizi kabla ya fasihi andishi, na kutokana na fasihi andishi hususan kazi za mwanzo za fasihi andishi kusemekana kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na fasihi simulizi (Mbele, 1982; Mulokozi, 1996), makala haya yanalenga kuichambua riwaya ya Uhuru wa Watumwa (1934) ili kuweza kuona namna tanzu mbalimbali za asili zinavyojitokeza katika riwaya hii na mchango wa tanzu hizo katika riwaya ya Kiswahili kwa ujumla. Uhuru wa Watumwa ni riwaya iliyotafitiwa na kuchambuliwa na wataalamu mbalimbali ambapo baadhi ya wataalamu hao (Senkoro, 1976; Mulokozi, 2000) wamebainisha kuwa ni riwaya ya kwanza ya Kiswahili.*


## 1.0 Utangulizi

Makala haya yana sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi wa masuala ya msingi. Sehemu ya pili inachambua tanzu za asili katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, na sehemu ya tatu inajadili mchango wa tanzu hizo katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* na riwaya ya Kiswahili kwa ujumla. Mwisho kuna hitimisho la mjadala mzima. Ni muhimu kufanya utafiti katika uga huu kwani tofauti na tanzu nyingine za fasihi, utanzu wa riwaya una uwezo wa kujumuisha wasifu wa tanzu nyingine lakini ukabakia kuwa na sifa zake kama utanzu (Bakhtin akinukuliwa na Wamitila, 2002). Ni jambo la kawaida kwa kazi za fasihi kuingiliana ili kuleta ladha fulani katika kazi hizo. Hii ni kwa sababu kazi moja ndefu yenye mtindo mmoja huweza kumchosha msomaji. Suala la kuchanganya tanzu katika kuunda kazi fulani ya fasihi, linaweza kuchukuliwa kama kipengele cha ubunifu.

Tunaweza kusema hakuna kazi ya fasihi inayoweza kujitegemea bila kuwa na mwingiliano na kazi nyingine au kuchota baadhi ya mambo kutoka katika kazi nyingine. Katika nadharia yake ya Mwingiliano Matini, Bakhtin akinukuliwa na Wamitila (2002) anaamini kuwa utanzu wa riwaya una uwezo wa kujumuisha wasifu wa tanzu nyingine na ukabakia na sifa zake kama utanzu. Kwa mfano, riwaya inaweza kuhusisha kipengele cha majibizano ambacho hutumiwa zaidi na tamthilia au ikahusisha ushairi na bado ikabakia kuwa riwaya. Anaendelea kusema kuwa utanzu huu una upekee kwa sababu unafyonza tanzu nyingine na kuzijumuisha katika muundo wake wa kipekee.

Suala la mwingiliano wa tanzu katika kazi za fasihi ni jambo ambalo halikwepeki, na ndio msingi wa maendeleo ya kazi za fasihi. Kwa mfano, tunapoangalia utanzu wa nyimbo katika fasihi simulizi, kwa hakika ndani yake utakuta methali au msemo au fumbo fulani. Kadhalika katika fasihi andishi,

utanzu mmoja na mwingine huingiliana. Kwa mfano riwaya nyingi hutumia mbinu mbalimbali za tamthilia, mathalani katika riwaya ya *Sitasahau Mv Bukoba* kuna matumizi mengi ya mbinu za tamthilia kama vile majibizano.

Tukiacha suala la tanzu kuingiliana ndani ya fasihi simulizi au fasihi andishi, pia kuna kuingiliana kwa fasihi andishi na fasihi simulizi. Kwa mfano, katika tamthilia za *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*, kuna matumizi ya mbinu za fasihi simulizi kama vile mbinu ya usimulizi ya kuanza na Paukwa...Pakawa.

Pamoja na hayo, fasihi simulizi inaonekana kuwa na athari kubwa katika fasihi andishi kuliko athari ya fasihi andishi katika fasihi simulizi. Hii ni kwa sababu fasihi simulizi ndiyo fasihi kongwe, na imekuwapo katika jamii tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Fasihi andishi iliingia baada ya kugundulika maandishi, ndipo ilipoanza kuchota yaliyokuwa katika fasihi simulizi kwa kutumia maandishi na kuwasilisha mambo mengine yaliyojitokeza katika jamii kwa njia ya maandishi.

Tanzu za asili ni miongoni mwa nyenzo za sanaa jadi hususan kumbowa fasihi simulizi, ambazo hujibainisha katika fasihi andishi ya Kiswahili kwa kutumia mbinu mbalimbali za kifani na kimaudhui.

Dundes (1965) anadai kuwa sanaa jadi/fasihi asilia huhusishwa moja kwa moja na wakulima au jamii ya vijijini na hata jamii za zamani sana. Mtaalamu huyu anaendelea kudai kuwa sanaa jadi haiwahusu watu wa kundi fulani bali kila kundi lina sanaa jadi yake, na kwamba jambo la muhimu ni kuwapo kwa mila na desturi wanazoziita za kwao. Hivyo, anaona kuwa kuna tanzu za asili zifuatazo: usanifu ujenzi, muziki, simulizi, sanaa ya vitendo au maonesho, pamoja na mila na desturi za jamii husika zinazohusu mavazi na vyakula.

Hata hivyo. kuna mwingiliano wa kiistilahi baina ya *sanaa jadi* na *fasihi simulizi*. Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakichanganya vipengele hivi. Kwa hakika si sahihi kusema sanaa jadi/fasihi asilia na fasihi simulizuzi ni visawe kwa sababu fasihi simulizi ni kipengele kimojawapo tu cha sanaa jadi ambacho kinahusu yale watu wasemayo kiutamaduni. Sanaa jadi ni dhana pana inayojumuisha fasihi simulizi ndani yake. Tofauti hizi zimewekwa bayana na Okpewho (1992).

Makala haya yanalenga kuichambua riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*. Riwaya hii imechambuliwa na kuhakikiwa na wataalamu mbalimbali, na inasemekana kuwa ni riwaya ya kwanza ya Kiswahili (Senkoro 1976, Mulokozi 2000). Kutokana na kwamba watunzi wa kazi za fasihi hawatungi kazi zao kutoka katika ombwe bali kutokana na yale yaliyomo katika jamii zikiwemo rasilimali za sanaa jadi zilizopo katika jamii husika. Ni dhahiri kuwa, riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* kama inavyosemekana kuwa riwaya ya kwanza ya Kiswahili, inaonekana kuchota ujumi mwingi wa sanaa jadi hususani kutoka katika fasihi simulizi ili kuweza kuikamilisha kazi hiyo. Katika makala yake ya "Oral Literature and the Writing Tradition", Mbele (1982) anasema:

> *One of the notable qualities of these early written versions of oral literature is their close affinity to the oral literature. There is a clear oral quality in the written versions.*

> Mojawapo ya nduni bainifu za maandishi ya mwanzo ya fasihi simulizi ni mahusiano yake ya karibu na fasihi simulizi. Kuna nduni simulizi bainifu katika maandishi ya mwanzo ya kazi za fasihi (Tafsiri yetu).

Mulokozi (1996) anasema, kazi za mwanzo za riwaya ziliathiriwa sana na sanaa jadi/tanzu za asili zilizokuwepo katika kipindi hicho, na miongoni mwa kazi alizotaja ni riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*.

## 2.0 Tanzu za Asili katika Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*

Katika sanaa jadi kama tulivyoona hapo juu, zipo tanzu mbalimbali, fasihi simulizi ikiwamo. Zipo tanzu nyingi za asili kama vile simulizi za watumwa, masimulizi ya kihistoria, masimulizi ya wasafiri, masimulizi ya kisira, ngano, hekaya, visasuli visakale, tendi, sira, insha, shajara, romansia, drama na kadhalika. Katika makala haya tunajadili baadhi tu ya tanzu hizo za asili. Hata hivyo, changamoto inayojitokeza ni kwamba, ni vigumu kuainisha tanzu za asili kutokana na kuingiliana kwa tanzu hizo kifani na kimaudhui. Uchambuzi wa tanzu za asili za fasihi simulizi katika riwaya hii ni kama ifuatavyo:

### 2.1 Simulizi za Watumwa

Kwa ujumla, riwaya hii ni simulizi ya watumwa (Mulokozi, 2003; Henry, 2011) inayoelezea tukio la biashara ya watumwa ilivyoendeshwa Afrika ya Mashariki na namna biashara hiyo ilivyokomeshwa (Senkoro, 1976). Simulizi za watumwa ni fasihi iliyochipuka kwa lengo la kuelezea uzoefu wa watumwa hususan Waafrika waliokuwa watumwa Uingereza na katika makoloni yake ya zamani ikiwamo Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kusini, Kanada, Karibiani na Afrika na kuhamasisha watu wachukie utumwa (Campbell (ht.), Henry 2011). Hii ndiyo athari kubwa inayojitokeza katika riwaya hii. Mzee Mambo Mbotela ambaye ndiye alikuwa mmoja wa watumwa anamsimulia mwanawe jinsi alivyotiwa utumwani pamoja na watumwa wengine kutoka maeneo mbalimbali ya Afrika ya Mashariki. Katika uk. 9-10, Mambo Mbotela anamsimulia mwanae kwa kusema:

> Hao wenyeji waliingiliwa na watu wasiowajua, nao walikuwa wakikamatwa na kufungwa... wako waliokamatwa mashambani, mitoni wakivua samaki, wako walioshikwa wakiwinda, malishoni, wengine ngomani, wengine visimani, hata nyumbani. Chiponda na watu wake pia walishikwa.

Pia, katika uk. 16, Mambo Mbotela anasema watumwa hao walitekwa nyara pande za bara za juu zaidi, nao walikuwa wa makabila mchanganyiko.

Mzee Mambo Mbotela anaendelea kumsimulia mwanae kuhusu suala zima la kutekwa, walivyosafiri kutoka katika maeneo yao ya asili kuelekea Pwani ya Afrika Mashariki, shida na tabu walizopata njiani ikiwa ni pamoja na kufanyiwa vitendo vya kikatili kama vile kuuawa ovyo, na namna walivyookolewa na Mwingereza na kupatiwa eneo jipya la kuishi la Kisauni. Katika uk. 9, Mambo Mbotela anamwambia mwanae:

> Basi mimi nitaanza kukueleza tokea mwanzo hadi mwisho. Nawe uwe na fahamu sawasawa, uje uwaeleze wanao, nao waeleze wana wao baadaye. Na ukiweza kuwaeleza walimwengu ni bora zaidi.

Alichofanya James Mbotela ni kuandika yale aliyosimuliwa na baba yake pamoja na kuongeza ubunifu katika kupangilia matukio hayo na wahusika kwa namna ambayo itamvutia msomaji. Akizungumza kuhusu kazi yake ya *Roots* (1976) ambayo ni simulizi ya watumwa yenye mkondo sawa na riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, Haley anasema kuwa kazi yake ni ya "*faction*" akimaanisha inajumuisha "*facts*" na "*fiction*", yaani "uhalisia" na "ubunifu". Hali hii ndiyo tunayoiona pia katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* ambapo mwandishi anaelezea tukio la kweli la biashara ya watumwa kifasihi.

Kazi yoyote ya fasihi lazima iwe na ubunifu, na tunapoongelea tukio la kweli kifasihi, hatuna budi kujumuisha kipengele cha ubunifu kwa sababu ndicho hasa kinachoipa ufasihi kazi hiyo, vinginevyo kazi hiyo itakuwa kama vitabu vingine vya taaluma mathalani vitabu vya hisabati, fizikia, jiografia, historia na kadhalika.

### 2.2 Masimulizi ya Kihistoria

Haya ni masimulizi ya matendo, mambo au matukio mbalimbali katika muktadha na wakati fulani wa kihistoria. Katika masimulizi ya kihistoria, tunaweza kupata masimulizi mbalimbali kulingana na matukio husika katika jamii husika, katika kipindi fulani cha kihistoria. Watunzi wengi wa kazi za fasihi huchota visa vyao katika jamii kwa kurejelea matukio muhimu ya kihistoria yaliyowahi kuimkumba jamii yao, na pengine kutoka katika jamii nyingine.

Yapo matukio mengine makubwa ambayo yamewahi kuikumba jamii yetu, na watunzi wameweza kutumia historia hiyo katika kuwapatia mawazo na visa katika kukamilisha kazi zao. Kwa mfano, tukio la kuzama kwa meli ya *Mv Bukoba* limetupatia riwaya ya *Sitasahau Mv Bukoba*, utandawazi nao umetupatia riwaya ya *Makuadi wa Soko Huria* na kadhalika.

Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* kwa hakika ni kisa kinachohusu historia ya biashara ya watumwa ilivyoendeshwa na Waarabu Afrika Mashariki karne ya kumi na tisa, na namna biashara hiyo ilivyokomeshwa. Ni riwaya inayohusu tukio la kweli la kihistoria kuhusu biashara ya watumwa. Jambo hili linaifanya riwaya

hii kuwa ya kihistoria. Mfano mwingine wa riwaya yenye masimulizi ya historia kuhusu biashara ya watumwa ni *Kwaheri Iselamagazi*.

### 2.3 Masimulizi ya Wasafiri

Masimulizi ya wasafiri ni jambo jingine linalojitokeza katika riwaya hii. Watumwa wanasimulia masaibu yaliyowapata katika safari zao tangu walipotekwa kutoka katika maeneo yao ya asili hadi walipofika katika nchi huru ya mateka Kisauni. Wanatoka kwao Mpanda kuelekea Pwani, na wengine wanasafirishwa kuelekea Bombay na Uingereza, lakini hatimaye wote wanakutana sehemu moja waliyoandaliwa kuishi ambayo ni Kisauni-Mombasa. Mzee Mambo Mbotela anamsimulia mwanawe kisa kizima cha safari yake ya utumwa na watumwa wenzake, tangu walipotekwa mpaka walipoanza maisha mapya Kisauni. Kadhalika katika riwaya hii kuna simulizi ndogondogo ambapo watumwa wanasimuliana kuhusu safari zao zilivyokuwa tangu wanatekwa mpaka wanapokutana Kisauni, kwa mfano, kuanzia uk. 10 ambapo mara baada ya kutekwa, safari inaanza kuelekea Pwani.

Kipengele hiki cha safari kinaweza kuchukuliwa kama motifu ya safari katika riwaya hii kutokana na kwamba kama tulivyokwishaona hapo juu, Mulokozi (2003) na Henry (2011) wanasema riwaya hii ni simulizi ya watumwa na katika motifu za msingi zinazojitokeza katika simulizi za watumwa ni motifu ya safari. Katika riwaya hii, motifu ya safari imetuwezesha kufahamu safari walizokuwa wakifanya watumwa na matatizo waliyopitia wakiwa njiani, hivyo kujenga maudhui ya riwaya hii.

### 2.4 Matumizi ya Hekaya

Hekaya ni hadithi ambayo ina visa vya kusisimua na kushangaza ambavyo si vya kawaida, na mara nyingi visa hivyo hufungamanishwa na mapenzi. Njogu na Chimerah (1999) wanasema hekaya ni hadithi ambazo zinatambulikana sana kwa ujanja wa mhusika mkuu. Mhusika mkuu huwa mtu, lakini huweza akawa mnyama pia. Katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, hekaya inajitokeza katika uk. 23-25 ambapo manyani wanawatafutia watumwa chakula na mizizi ambayo iliwasaidia watumwa hao kama dawa ya magonjwa yaliyokuwa yakiwasumbua, pia kuwaongoza watumwa katika njia sahihi ya kuelekea Pwani. Katika uk. 25 mwandishi anasema:

> Manyani walitambua ya kwamba safari inaanza basi mahali pa kuchukua pembe kama zile zilizochukuliwa na watumwa, wao walichukua mapande ya miti tu, kuwaigiza hao watumwa. Nao ndio waliowaongoza njia.

Pamoja na utumizi wa hekaya katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, riwaya ya Kiswahili imekuwa ikichota mbinu za kifani na kimaudhui kutoka katika fani hii

ya hekaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Adili na Nduguze* kuna visa vya kusisimua na kushangaza ambavyo si vya kawaida.

## 2.5 Matumizi ya Ngano

Ngano ni hadithi fupi simulizi. Balisidya (1987) anasema, ngano ni hadithi za "paukwa pakawa... wakaishi raha mustarehe" na aghalabu huwa na nyimbo. Anaendelea kusema kuwa, huwa na wahusika wa aina mbalimbali kama vile wadudu, wanyama, binadamu, mizimu, na miungu na viumbe visivyo na uhai kama vile mawe, miamba na kadhalika. Mulokozi (1996) anasema ngano ni hadithi za kubuni na nyingi zinahusu wanyama, lakini zipo pia zinazohusu wanadamu, mazimwi, majini na malaika. Dhamira huhusu mgongano kati ya wema na uovu, choyo, tamaa na motifu kama ya safari, zimwi lafi, bibi kizee, mama wa kambo, siri ya hazina iliyofichwa na kadhalika. Njogu na Chimerah (1999) wanasema ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni. Wamitila (2003) anasema ngano ni hadithi ya kale ambayo ni moja kati ya tanzu maarufu za fasihi simulizi.

Kwa hakika, katika riwaya hii kuna simulizi kadhaa za kingano. Kwa mfano katika uk.1-8, Mbotela anamsimulia mwanawe kuhusu kwao Mpanda. James alisimuliwa kuhusu maisha ya Mpanda yalivyokuwa, vyakula walivyokula na utamaduni wao ulivyokuwa. Hadithi nyingine fupi tunaipata katika uk. 23-25 kuhusu manyani. Mifano mingine ya kazi za Kiswahili zenye visa vya kingano ni *Kusadikika,* na *Adili na Nduguze*. Hii inamaanisha kuwa tanzu za asili na hususan ngano, zimechangia kwa kiasi kikubwa kifani na kimaudhui katika kuvyaza riwaya ya Kiswahili.

## 2.6 Matumizi ya Kisasuli

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996), kisasuli, kisasili, cha usuli' huelezea chimbuko/asili ya kitu kwa lengo la kuburudisha zaidi, na hii inatokana na kile kinachoelezewa kukosa uzito wa kukifanya kiaminiwe kuwa cha kweli kama ilivyo kisasili. Utanzu wa kisasuli nao tunauona katika uk. 8, ambapo James anasimuliwa na baba yake kuhusu suala la kumbikumbi kupigiwa mbiu. Mzee Mambo Mbotela anasema:

> Wadudu hao si wazuri wakikamatwa ovyo tu, mtu huwa kiziwi. Tena mwanadamu wa kwanza alitoka vichuguuni, basi vichuguuni mna vizuka, hamwendewi ovyo.

Kutokana na kisasuli hicho kukosa uzito, James alipokuwa akisimuliwa alicheka sana kwa sababu hakuamini kama hayo aliyosimuliwa yalikuwa ya kweli.

**2.7 Masimulizi ya Kisira**

Haya ni masimulizi yanayosimuliwa kuhusu maisha ya mhusika au wahusika tangu wanapozaliwa hadi pale wanapokomea. Kwa upande wa riwaya, kutokana na fani hii ya masimulizi ya kisira, waandishi mbalimbali huandika kazi zao nyingine zikiwa zile zinazohusu maisha yao au zinazohusu maisha ya watu wengine, na hivyo kupatikana kwa mkondo wa riwaya za kisira. Masimulizi ya kisira yanajitokeza ijapokuwa kwa ufupi katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*. James Mbotela anaelezea maisha ya baba yake tangu alipokuwa Mpanda, maisha yake ya utumwa na mpaka alipofariki. Matumizi ya sira yanajitokeza pia katika kazi nyingine za riwaya hata za hivi karibuni. Baadhi ya kazi hizo ni pamoja na *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, *Kurwa na Doto*, *Rosa Mistika*, *Kichwamaji*, *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Kwaheri Iselamagazi* na kadhalika.

**3.0 Mchango wa Tanzu za Asili katika Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* na Riwaya ya Kiswahili kwa ujumla**

Kutokana na matumizi makubwa ya tanzu za asili katika riwaya ya Kiswahili na kama tulivyoona katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* katika sehemu iliyotangulia, ni wazi kwamba tanzu hizi za asili zina mchango mkubwa katika kukua kwa riwaya ya Kiswahili. Kipengele hiki kinaeleza mchango huo kama ifuatavyo:

**3.1 Mtindo wa Usimulizi wa Kinathari**

Tanzu za asili hususan masimulizi/hadithi zina usimulizi wa lugha ya kinathari. Kazi za riwaya kwa ujumla, *Uhuru wa Watumwa* ikiwamo, zimekuwa zikitumia mtindo huu wa usimulizi wa kinathari kuelezea matukio mbalimbali yaliyomo katika jamii. Inafahamika kwamba awali zilikuwapo simulizi za kishairi kama vile *Swifa ya Mwanamanga*, utendi wa *Fumo Liyongo*, *Tambuka* na kadhalika, lakini kutokana na kuwapo kwa tanzu za asili zenye usimulizi wa kinathari kama tulivyoona katika uchambuzi wetu, kazi za riwaya zilifuata mtindo huo, sifa ambayo inatofautisha riwaya na tanzu nyingine za fasihi andishi ambapo lugha ya mkato inapambanua ushairi na lugha ya mazungumzo inapambanua tamthilia.

**3.2 Kuzuka kwa Riwaya ya Kihistoria**

Katika tanzu simulizi, watu walikuwa na huwa wanasimuliana mambo na matukio kadha wa kadha, hasa matukio makubwa na mazito ambayo yameikumba jamii yao. Kwa mfano, ni jambo la kawaida kukuta watu wakisimuliana kuhusu tukio la kuzama kwa meli ya *Mv Bukoba* lililoikumba jamii ya Watanzania mwaka 1996. Masimulizi kama hayo pamoja na ubunifu wa msanii vimeweza kutupatia riwaya za kihistoria. Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* inahusu tukio la kweli la kihistoria la biashara ya watumwa, namna ilivyoendeshwa na namna ilivyokomeshwa Afrika Mashariki. Hili linaifanya riwaya hii kuwa ya kihistoria kutokana na kuongelea mambo halisi yaliyotokea katika jamii. Kazi nyingine za riwaya zenye mkondo

huu ni pamoja na *Uhuru wa Watumwa, Kwa heri Iselamagazi, Sitasahau Mv Bukoba* na kadhalika inaeleza matukio ya kweli ya kihistoria yaliyowahi kutokea katika jamii.

### 3.3 Maudhui Changamani

Fasihi simulizi hufungamana na utamaduni wa jamii, na hubadilika kadiri jamii inavyobadilika kwa kuzingatia vipindi tofautitofauti vya kihistoria. Kutokana na jamii mbalimbali kuingiliana hususan kwa sababu za kibiashara, utamaduni wa jamii hizo nao huathiriana. Kutokana na kwamba fasihi andishi na kwa mujibu wetu, riwaya, huchota maudhui yake kutoka katika jamii, riwaya hiyo itakuwa na maudhui changamani. Kwa mfano, katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* kuna maudhui ya Kikristo, ya kijadi na ya Kiislamu ambayo yanatokana na mwingiliano wa jamii ya Waswahili wa Waarabu na Waingereza. Kazi nyingine zinazochanganya maudhui namna hii ni kama vile *Utu Bora Mkulima, Kufikirika, Kusadikika, Rosa Mistika* na kadhalika. Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa riwaya nyingi za Kiswahili zina maudhui changamani kwa maana kwamba maudhui katika kazi hizo hayajikiti katika jambo moja tu bali yanachambua mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa mwigiliano wa tamaduni mbalimbali, dini, lugha, elimu na nyanja zote kwa ujumla.

### 3.4 Matumizi ya Ontolojia Changamani

Ontolojia ni mtazamo wa jamii kuhusu maisha na kuwapo kwa mwanadamu na ulimwengu kwa ujumla. Katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* kuna ontolojia ya Kizungu, Kiarabu na Kiafrika. Mataifa yote haya matatu kila moja lina ontolojia yake, na tunaona namna ontolojia ya Kiafrika inavyotupiliwa mbali na namna Waafrika wanavyoanza kuyatazama maisha kwa namna tofauti ikiwa ni pamoja na kubadili mitazamo yao kuhusu dini zao kwamba wanaanza kuziona ni za kishenzi. Pia, suala la maisha lilithaminiwa sana na Waafrika ukilinganisha na Waarabu ambao walikuwa hawathamini maisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* uk. 11, Waarabu wanaua watu ovyo. Chaliwali anasema, "Msiponyamaza nitawakatilia mbali vichwa vyenu kwa upanga. Angalieni jinsi nilivyomtenda huyu jamaa yenu, nanyi mkiniasi nitawatenda vilevile". Katika *Janga Sugu la Wazawa* kuna ontolojia ya Kiafrika, Kizungu na Kiarabu. Bugonoka alipewa jina la bibi yake, jambo ambalo ni ontolojia ya Kiafrika ya ujamiishaji wa kiduara. Kadhalika katika *Rosa Mistika* kuna ontolojia ya Kiafrika na ya Kizungu ambapo wazazi wake Rosa wanawakilisha ontolojia ya Kiafrika ilhali Rosa anachanganya ontolojia ya Kiafrika na ya Kizungu.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, kuna uchanganyaji wa ontolojia ya jadi na ya dini ya Kiislamu. Kazi nyingine zinazochanganya ontolojia ni pamoja na *Adili na Nduguze, Rosa Mistika, Nagona, Mzingile*, na nyingine.

### 3.5 Mtindo wa Lugha

Lugha inayotumika katika tanzu za asili ni lugha nyepesi ya masimulizi inayoeleweka. Ukiacha riwaya za usasa za majaribio zenye kutumia lugha ya picha na ishara kwa kiasi kikubwa, riwaya nyingi za Kiswahili, *Uhuru wa Watumwa* ikiwemo, zimeiga mtindo huu wa lugha nyepesi inayoeleweka. Ifahamike kwamba zipo riwaya chache ambazo zimechanganya lugha nyepesi na ya picha na ishara kwa kiasi kidogo, lakini kuchanganya huku si sababu ya kutokueleweka kwa kazi hizo endapo itatokea kazi hizo kutoeleweka.

Katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* kwa mfano, kuna uchanganyaji mdogo wa lugha, na hii inatokana na ama mwingiliano wa tamaduni uliokuwapo katika jamii. Kwa mfano, katika uk. 34, kuna maneno ya lugha ya Kiingereza *oh dear! oh dear!* na katika uk. 36 kuna maneno *there it is! there it is!*

Uchanganyaji wa lugha tunaweza kuuona pia katika riwaya ya *Bwana Myombokere na Bibi Bugonoka*. Mwandishi katika riwaya hii ametumia lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikerewe.

### 3.6 Wahusika na Namna Wanavyochorwa

Katika tanzu za asili wahusika wanaotumika ni binadamu, vitu na viumbe mbalimbali. Wahusika hao huchorwa kwa namna ambayo kila mmoja anabeba ujumbe fulani kwa jamii. Kwa mfano, zilikuwapo hadithi mbalimbali zilizosimuliwa kwa lengo la kutoa maadili, kuelimisha, kusifu, kupongeza na kadhalika kulingana na muktadha fulani katika jamii, na tunaona kuwa wahusika hao ndio waliobeba maudhui hayo. Namna hii ya uchoraji wa wahusika katika tanzu za asili inatumika pia katika kazi mbalimbali za fasihi, na kwa mujibu wetu kazi za riwaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* wahusika wamechorwa kwa namna ambayo wanasawiri hali halisi iliyokuwapo katika jamii ya utumwa na biashara ya watumwa. Pia, kuna matumizi ya wahusika binadamu na wanyama.

### 3.7 Muundo, Mtindo wa Hadithi Usimulizi na Msuko wa Matukio

Kila tanzu simulizi ina muundo na mtindo wake. Kwa mfano, ngano inatumia muundo wa moja kwa moja/sahili na ina mtindo wake wa usimulizi. Hekaya zina mtindo wa hadithi ndani ya hadithi au kuchanganya mitindo tofautitofauti ya usimulizi. Katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* na riwaya nyinginezo za Kiswahili, kuna mtindo huu wa hadithi ndani ya hadithi. Katika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa*, hadithi kuu, inahusu suala la biashara ya watumwa ilivyoendeshwa na namna ilivyokomeshwa pwani ya Afrika Mashariki. Ndani ya hadithi hii kuu tunapata hadithi nyingine ndogondogo kama vile hadithi ambazo watumwa walikuwa wakisimuliana kuhusu safari zao za utumwa zilivyokuwa, pia kuna hadithi ya manyani ambao waliwasaidia watumwa kuangua matunda njiani na kuwaonesha njia ya kuelekea pwani huku wakiwa wamejitwika magogo ya miti mithili ya mizigo waliyokuwa wamebeba watumwa vichwani mwao na kadhalika.

Kuhusu msuko wa matukio, tanzu za asili kama vile ngano zina muundo sahili. Muundo huu tunauona katika baadhi ya kazi za riwaya ya Kiswahili kama vile riwaya ya *Uhuru wa Watumwa, Kusadikika, Kufikirika, Adili na Nduguze, Mzimu wa Watu wa Kale* na kadhalika. Katika kazi hizi kuna mtiririko sahili wa matukio ambapo mwisho wa tukio moja unakuwa mwanzo wa tukio jingine.

**4.0 Hitimisho**

Ukongwe wa fasihi simulizi umeweka msingi wa fasihi andishi ambapo watunzi wengi wa fasihi andishi wamekuwa wakichota mambo mbalimbali ukiwemo ujumi wa fasihi hii kongwe na kuutumia katika kazi zao. Kwa ujumla, tanzu hizi za asili; zinajitokeza si katika kazi za mwanzo tu za fasihi andishi, bali pia katika kazi za sasa, na huenda tanzu hizo zinajitokeza zaidi katika kazi za sasa kuliko zilivyojitokeza katika kazi za mwanzo. Ni jukumu la wanataaluma kuendelea kuchunguza namna tanzu za asili na sanaa jadi zinavyoathiri si riwaya tu bali fasihi andishi kwa ujumla, huenda kikagundulika kitu kipya kitakachoendeleza uwanja huu wa fasihi.

## Marejeo


Balisidya, M.L. (1987). "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi", katika *Mulika* Na. 19. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur 2-10.

Chachage, C.L. (2002). *Makuadi wa Soko Huria*, Dar es Salaam: E&D Limited.

Campbell, D.M. (ht.). "The Slave Narrative", katika *Literary Movements*. Department of English, Washington State University, imesomwa 28, Novemba, 2010: http://www.wsu.edu/-campbelld/amlit/slave.htm.

*Farsy, M.S. (1960). Kurwa na Doto, Nairobi: EALB.*

Haley, A.A.P. (1976). *Roots:The Saga of an American Family*. New York: Doubleday.

Henry, G. (2011). "Riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* katika Muktadha wa Simulizi za Watumwa". Tasinifu ya Umahiri katika Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Hussein E. (1976). *Jogoo Kijijini na Ngao ya Jadi*, Nairobi:Oxford University Press.

Katalambula, F.H. (1965) *Simu ya Kifo*, Nairobi: EALB.

Kezilahabi E. (1974). *Kichwamaji*, Dar es Salaam: East African Publishing House.

_________ (1975). *Dunia Uwanja wa Fujo*, Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

_________ (1975). *Rosa Mistika*, Dar es Salaam: DUP.

_________ (1990). *Nagona*, Dar es Salaam: DUP.

_________ (1991). *Mzingile*, Dar es Salaam: DUP.

Kijumwa, M. (1973). *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Dar es Salaam: TUKI.

Kitereza, A. (1980). *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka: Ntulanalwo na Bulihwali,* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mapalala B. (1992). *Kwaheri Iselamagazi,* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa Watumwa.* London: Sheldom Press.

Mbele, J. (1982). "Oral Literature and the Writing Tradition", katika *Kiswahili* Juz.49 Na. 1. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur 1-8.

Mlacha, S.A.K. (1985). "Wahusika katika Riwaya za Kiswahili Tanzania" katika *Mulika* Na.17. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur 29-45.

Mulokozi, M.M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili,* Dar es Salaam: KAUTTU.

Mulokozi, M.M. (2000). "Utamaduni wa Usomaji Tanzania", katika *Mulika* Na. 26, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur 75-91

Wamitila, K.W. (2003). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix Publications Ltd.

Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity,* Bloomington na Indianapolis: Indiana University Press.

Robert, S. (1952). *Adili na Nduguze,* London: Macmillan.

_________ (1966). *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini,* Dar es Salaam: Nelson.

_________ (1968). *Utu Bora Mkulima,* Nairobi: Nelson & Sons Ltd.

_________ (1990). *Kusadikika,* Nairobi: Evans Africa.

Senkoro (1976). "Utamaduni katika Riwaya ya Kiswahili", katika *Kiswahili* Juz. 46/2. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: kur 74-82.

Simango, N. (2009). *Sitasahau MV Bukoba,* Dar es Salaam: E&D Vision Publishing Limited.